

Dondoo za mukutano wa Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam
18 Julai 2009

Waliohudhuria

Athumani Mussa Kitemo

Juma Ali Salehe Jongo

Mohammed Samwely

Beda John Mkusu

Paulo Atibu Hatibu

Abdul H Mwaibambe

Rahma Ali

Shamte J Kisoma

Ally Salum

Rajabu S Mkialiko

Filbert Mbecha

Saidi Brashi

Bashiri Rashidi

Hamadi Hatibu Bwaja

Elaine Baker

Selion Elieskia

Edgar R Paulo

Kibwana Mohammad Msiga

Mukutano wa Baisikeli, Nairobi

Filbert aliandika repoti kuhusu mukutano wa Nairobi na Elaine atachapa. Elaine aliscan photos na ataweka repoti kwenye website.

Mukutano wa usalama barabarani, Dar es Salaam

Elaine alichapa reporti Hamadi aliyoandika. Elaine ataweka repoti kwenye website.

Mradi wa Wamba

Elaine aliandika barua ya shule ya Mbondole. Mwalimu wa Mbondole atakuja ofisin kwetu jumatatu kuchukua na kuongea kuhusu mafunzo saa nne na nusu. Hamadi na Juma watakuwepo ofisini kuongea naye.

Msafara

Filbert alipeleka proposal Zain. Hamadi alipeleka proposal Serengeti. Juma alipeleka proposal balozi za Ireland, UK, Netherlands, Sweden, Denmark. Paulo alipeleka kampuni ya guta. Kibwana alipeleka Zantel. Elaine ataleta nakala zingine za proposal na barua pia ili tufuatalie tena na mashirika haya.

Kutafuta mikutano

Elaine aliandika barua za kutafuta mikutano na Meya wa Dar es Salaam, Waziri wa Miundombinu, Madiwani ya Jiji, Komanda James Kombe, na pia kualika watu wa serikali ya mtaa. Wanachama wengine walisahihisha barua. Elaine ataweka mabadilisho na kumpa Juma barua ziwe ofisini. Abdul atapeleka kwa serikali ya mtaa. Filbert atapeleka kwa Waziri wa Miundombinu na nakala ya barua ya meya kwa diwani Lupilya. Saidi atapeleka kwa Komanda Kombe na ofisi ya Meya.

Uchaguzi wa 2010

Elaine alisoma ilani za uchaguzi za 2005 za TLP na CCM na usalama barabarani na masuala ya baisikeli hayapo. Elaine aliandika barua kwa wenyejiti wa vyama kuwaauliza ilani za uchaguzi zinaandikwa lini na vipi sisi tunaweza kuchangia mawazo, na wanachama walisahihisha. Edgar atapeleka barua CCM na Paulo atapeleka barua TLP, CUF, CHADEMA na NCCR-Maguezi.

Marekebisho madogo madogo ya barabara

Elaine alipendekeza tuwe na fomu ya kutoa repoti ya matatizo ya barabara na watu wanaovunja sheria.

Mafunzo ya Lugha

Mwalimu alisema watu 8 walihudhuria mafunzo ya kiingereza leo asubuhi. Mafunzo yataendelea kesho jioni.

Website

Elaine alisema kwamba kampuni ya yahoo-geocities walitangaza kwamba wanafunga huduma zao za geocities website. Kwanza huduma ilikuwa bure halafu ilikuwa \$5 kwa mwezi ambayo Elaine analipa kutoka hela zake. Basi website yetu intafutwa na lazima tuhamishe sehemu nyingine. Alipata taarifa kutoka University Computing Centre kwamba tunaweza kupata anwani ya www.uwaba.or.tz (ambayo ni bora kuliko anwani ya .com) na pia kuweka website yetu kwa Tsh 142,000 kwa mwaka. Wanachama walikubali kulipe kiasi hichi.

Kodi ya ofisi

Wakati wa wiki Juma na Elaine walienda benki walichukua Tsh 200,000 wakalipa kodi ya ofisi kwa Juma Chibaya (alikuwa ameshapata Tsh 40,000 kama advance). Alisaini mkataba. Tumelipa kodi ya ofisi sasa mpaka tarehe 1 mwezi wa nane 2010.

Hela na guta

Filbert alibadilisha mchango wa \$40 na alipata Tsh 52,400. Filbert, Edgar na Mejah walirudisha Tsh 105,000 ya advance ya Tsh 150,000, bado wanadaiwa Tsh 45,000. Dereva wa guta hajalipa sasa anadaiwa Tsh 29,000. Elaine alipewa Tsh 25,800 ambayo alidai. Juma alipewa Tsh 750 alitumia kufanya photocopy ya proposal ya msafara. Hela inayobaki ni Tsh 130,850 na Elaine alichukua ili alipe website.

Mambo mengine

Tutapata reporti ya Tanga Dominata akirudi.

Bado tunasubiri taarifa ya msamaha wa kodi kabla ya kuendelea na mradi wa Re-Cycle.

Kuhusu Fasta courier cooperative – tutakutana na Bwana Bukuku Mejah akiwepo.

Mejah anatayarisha CD cover kwa ajili ya wimbo.

Tutakubali siku ya uchaguzi wa kamati Mejah akiwepo.

Edgar alisema mwanafunzi mmoja wa mafunzo ya Magomeni alifariki ghafla alikuwa na umwa.

Elaine alitangaza kwamba ataolewa tarehe nane nane na ataalika baadhi ya wanachama wa UWABA, lakini siyo wote kwa sababu ya nafasi.